**HOTUBA YA MKUU WA CHUO CHA ARDHI MOROGORO**

**NDUGU JUSTO LYAMUYA ILIYOTOLEWA KWENYE MAHAFALI YA THELATHINI NA TANO YA CHUO CHA ARDHI MOROGORO TAREHE 24-03-2017**

**Mgeni Rasmi,**

Kwa niaba ya Jumuiya ya Chuo cha Ardhi Morogoro, na kwa niaba yangu binafsi, ninayoheshima kukukaribisha Dkt. Moses Kusiluka naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Wageni waalikwa wote katika Mahafali ya Thelathini na Tano ya Chuo cha Ardhi Morogoro.

**Mgeni Rasmi,**

Wanajumuiya ya Chuo cha Ardhi Morogoro wanafurahia jinsi unavyotusaidia katika mambo mbalimbali ya chuo kama vile uboreshaji wa Muundo wa Utumishi, uandaaji wa Mpango Mkakati wa miaka mitano n.k.

**Mgeni Rasmi,**

Aidha nawapongeza Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi ya Chuo kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kusimamia na kutushauri. Nawashukuru viongozi wa Serikali ngazi ya Mkoa na Wilaya, Idara za Serikali, Mashirika ya Umma yaliyopo Morogoro, Wazabuni, Majirani, Wazazi, Ndugu, Marafiki na wageni wote mliokuja

kushiriki nasi mahafali haya. Kwani sherehe ni watu na watu ndiyo ninyi wageni wote **Asanteni na karibuni sana.**

**Mgeni Rasmi,**

Chuo cha Ardhi Morogoro kinao usajili kamili (Full Registration) pamoja na ithibati kamili (Full accreditation) ya Baraza la Taifa la Elimu a Ufundi yaani 'NACTE'. Usajili na ithibati zinafanya Chuo kuwa na uwezo wa kuanzisha kozi mbalimbali zenye tija kwa Taifa.

Kwa kuzingatia hilo, Chuo kimepeleka 'NACTE' mitaala ya kozi mpya ya Mipango Miji, kwa ngazi za cheti na Stashahada. Mitaala hii inazingatia zaidi utendaji yaani "Competence-Based Curricula". Ni imani yangu kuwa Wizara ya Ardhi na wadau wa elimu watasaidia kozi hii kuanza kwa haraka ili kutimiza lengo la kila kipande cha Ardhi nchini kupangwa na kupimwa hivyo kusaidia katika kukuza Uchumi wa Viwanda.

**MAFANIKIO;**

**Mgeni Rasmi,**

- Mwaka 2012 Chuo kimesomesha watumishi wake wanne, wawili wamemaliza na kutunukiwa shahada ya kwanza na wawili shahada ya Uzamili.

- Mwaka 2013 Chuo kimesomesha wakufunzi wawili (2) ngazi ya shahada ya Uzamili na watumishi wengine (supporting staff) watatu ngazi ya stashahada.

- Mwaka 2015-2017 Chuo kilisomesha wakufunzi wawili (2) ngazi ya shahada ya Uzamili na watumishi wengine watatu ngazi ya cheti na stashahada. Mtumishi mmoja bado anaendelea na masomo ya stashahada ambayo atahitimu mwaka 2018.

- Chuo kimefanikiwa kufanya mapitio ya nyaraka mbalimbali zikiwemo ya Muundo wa Taasisi, Muundo wa Maendeleo ya Watumishi (Scheme of Service) na Mpango Mkakati wa chuo.

- Chuo kimefanikiwa kuanza taratibu za kuandaa tovuti ya chuo kwa ajili ya kuboresha mawasiliano kwa watu wake na umma kwa ujumla.

**Mgeni Rasmi**,

Katika Mahafali ya thelathini na tano kuna jumla ya wahitimu **171**. Kati yao **35** ni wa kike na **136** ni wa kiume. Wahitimu wa Stashahada ya Jiomatikia (NTA 6 Ordinary Diploma in Geomatics) ni **60**, wahitimu wa cheti (NTA 5-Technician Certificate in Geomatics) ni **70** na cheti cha awali (NTA 4-Basic Technician Certificate in Geomatics) ni **41**. Chuo kinawahamasisha wasichana kujiunga na mafunzo ya Upimaji Ardhi kwani Chuo hutoa kipaumbele cha kwanza kwa wasichana wanaoomba kujiunga. Toka mwaka **1983** hadi **2015** kuna jumla ya wahitimu **905** wa cheti kati yao

hao **112** ni wa kike. Wahitimu wa Stashahada tangu ilipoanza mwaka **2003** ni **500** na kati ya hao **60** ni wa kike.

**Mgeni Rasmi**,

Chuo cha Ardhi Morogoro kilianza mwaka 1978 kikiwa tawi la Chuo cha Ardhi Dar-es-salaam. Chuo kimeendelea kufanya maboresho katika kozi na mitaala kukabiliana na changamoto za kitekinolojia na mahitaji ya soko.

Changamoto kubwa inayokikabili Chuo ni;

- Uendelezaji wa eneo la ekari 33 (hekta 9) lililoko Mlimakola katika Manispaa ya Morogoro kwa ajili ya kupanua wigo wa mafunzo, miundo mbinu na kuongeza udahili wa wanafunzi. Mpango huu uwatawezekana tu iwapo Serikali kupitia Wizara yako Mgeni Rasmi itatoa kipaumbele katika ujenzi wa eneo hilo.

- Madeni ya wazabuni na ufinyu wa bajeti umechangia kuwepo kwa upungufu wa vifaa vya kufundishia hivyo kupunguza kasi ya chuo kukua na kudahili wanafunzi wengi ingawa maombi ya kujiunga chuo hupokelewa zaidi ya 400. Kutokana na hali hiyo chuo kinadahili wanafunzi 80 tu.

- Pia Chuo kina upungufu mkubwa wa vifaa vya kufundishia mfano; tuna seti 1 tu ya GPS, Total station 6 ( kati ya hizo tatu ni mbovu). Upungufu huu wa vifaa unaathiri sana mafunzo kwa njia ya vitendo. Tunaomba

vifaa vitakavyonunuliwa chini ya mkopo wa Benki ya Dunia ukifikirie Chuo kupata baadhi ya vifaa.

- Aidha chuo kinazo changamoto zingine kama usafiri (Chuo kina gari moja tu), tunaomba ukisaidie chuo kipate gari jipya

- Baadhi ya wanafunzi kutokulipa ada kwa wakati.

- Kutokuwepo wasaidizi maeneo ya uhasibu na Ugavi.

- Upungufu wa vitabu, Uchakavu wa miundo mbinu mfano majengo na mabomba ya maji.

- Ujenzi wa Maktaba kutokamilika kwa muda mrefu na uhaba wa mabweni kwa wanafunzi.

**Mgeni Rasmi,**

Naomba nihitimishe hotuba yangu kwa kukushukuru tena kwa kukubali kuwa Mgeni Rasmi katika mahafali haya. Nawashukuru Wajumbe wa Bodi kwa kusimamia vyema shughuli za Chuo hiki, nawashukuru wageni wote waalikwa na wahitimu. Sina budi pia kuwashukuru wakufunzi wote pamoja na jumuiya nzima ya Chuo cha Ardhi Morogoro kwa mchango wao katika kutoa huduma na kufikia mafanikio makubwa tunayoyasherekea leo hii. Naishukuru kamati ya mahafali ambayo katika kipindi kifupi imefanya kazi kubwa na nzuri.

Mwisho nakuomba Mwenyekiti wa Bodi uchukue fursa hii kutoa hotuba yako na hatimaye umkaribishe Mgeni Rasmi aongee na hadhara hii.

**Asanteni sana kwa kunisikiliza.**